

MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA DESEMBA, 2017 NA MWELEKEO WA JANUARI, 2018

Dondoo za Januari, 2018

Taarifa hii inatoa muhtasari wa hali ya viashiria vya hali ya hewa na mwenendo wa mvua katika mwezi wa Desemba, 2017 na mwelekeo wa viashiria na hali ya mvua kwa mwezi Januari, 2018 nchini.

- a) Maeneo mengi ya nchi yameendelea kupata mvua za 'Vuli' na 'Msimu', hata hivyo maeneo ya Nyanda za juu kaskazini mashariki na kati mwa nchi hususani mkoa wa Dodoma yamekuwa na mtawanyiko hafifu sana wa mvua.
- b) Ukanda wa mvua (ITCZ), unatarajiwa kuendelea kusogea kuelekea maeneo ya kusini, hivyo kusababisha vipindi vya upungufu wa mvua katika maeneo ya kusini mwa nchi. Maeneo ya Pwani ya kaskazini pamoja na Nyanda za juu kaskazini mashariki yanatarajiwa kuwa na uwezekano mdogo wa mvua za nje ya msimu.

1.0 MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA DESEMBA, 2017 NA MATAZAMIO KWA MWEZI JANUARI, 2018.

1.1 MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA DESEMBA, 2017

Vipindi vichache vya mvua kubwa vimeripotiwa katika kipindi cha mwezi Desemba, 2017 katika baadhi ya maeneo ya Kibondo, Zanzibar, Matangatuani, Pemba, Bukoba, Mahenge na Songea. Hata hivyo maeneo ya Pwani ya kusini (Naliendele na Mtwara) yameongoza kwa kuripoti mvua nyingi zaidi.

2.0 MATAZAMIO JANUARI, 2018

2.1 MIFUMO YA HALI YA HEWA

Maeneo ya kati ya Kitropiki ya bahari ya Pasifiki yanatarajiwa kuendelea kuwa na joto la bahari la chini ya wastani na joto la bahari la wastani katika eneo la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi linatarajiwa. Hali hii inatarajiwa kuendelea kupunguza mvua hususan katika maeneo ya Pwani ya kaskazini. Hali ya joto la bahari la wastani hadi chini ya wastani eneo la pwani ya Angola, inatarajiwa kuendelea kuleta upepo wenye unyevunyevu kutoka magharibi kuelekea katika maeneo ya magharibi mwa nchi, hivyo kusababisha mvua na ngurumo katika baadhi ya maeneo.

Ukanda wa mvua (ITCZ), unaendelea kusogea kuelekea maeneo ya kusini, hivyo kusababisha upungufu wa mvua katika maeneo kusini pamoja na Pwani ya kusini.

2.2 MWELEKEO WA MVUA KWA MWEZI JANUARI, 2018

Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Pwani, Dar es Salaam, maeneo ya kaskazini mwa mkoa wa Morogoro pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba): Kunatarajiwa kuwa na uwezekano mdogo wa vipindi vichache vya mvua za nje ya msimu.

Nyanda za juu kaskazini mashariki (Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara): Maeneo haya yanatarajiwa kuwa makavu kwa ujumla, hata hivyo kuna uwezekano mdogo wa kuwa na mvua za nje ya msimu.

Kanda ya ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Mara na Simiyu): Vipindi vichache vya mvua na ngurumo vinatarajiwa katika maeneo machache.

Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora): Vipindi kadhaa vya mvua na ngurumo vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo.

Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida): Vipindi kadhaa vya mvua na ngurumo vinatarajiwa katika maeneo machache.

Nyanda za juu kusini magharibi (Mikoa ya Rukwa, Njombe, Iringa, Mbeya pamoja na maeneo ya kusini mwa mkoa wa Morogoro):

Vipindi vingi vya mvua na ngurumo vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo.

Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi): Vipindi kadhaa vya mvua na ngurumo vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo.

Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma): Vipindi kadhaa vya mvua na ngurumo vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo.

Imetolewa na; **MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA**